

(52). Harun Ajenga Jumba La Kifalme

Harun alijengea jumba la kifalme, na ilipokuwa tayari, siku moja alikuwa darini akiangalia mandhari yaliyomzunguka. Mara alimuona Bahlul akiangalia jengo hilo jipya.

Harun alimwita kwa kusema: "Ewe Bahlul! Ninalo ombi, je unaweza kuniambia maneno mazuri mno kwa ajili ya Jumba hili langu la kifalme?"

Bahlul alitafuta mkaa na aliandika kwa haraka juu ya ukuta wa Jumba hilo maneno yafuatayo: "Umeinua ardhi ambapo umeipotosha *Din*. Iwapo umeijenga kwa fedha za Umma, basi kwa hakika umedhulumu na kwa hakika Mwenyezi Mungu hawapendi madhalimu."